# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MAAMUZI YA TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA KUREJESHA UDAHILI, KUENDELEA KUSITISHA UDAHILI WA WANAFUNZI WAPYA, NA KUFUTA USAJILI KWA BAADHI YA VYUO VIKUU NCHINI

### 1.0 Utangulizi

Itakumbukwa kwamba kati ya mwezi Oktoba 2016 na Januari 2017 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ilifanya ukaguzi maalum wa kitaaluma kwa taasisi zote 64 za vyuo vikuu, vyuo vikuu vishiriki, na vituo vya vyuo vikuu.

Lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa elimu ya juu itolewayo inakidhi viwango vya ubora kitaifa, kikanda na kimataifa. Matokeo ya ukaguzi yalibainisha kasoro mbalimbali katika uendeshaji wa vyuo vikuu nchini. Vyuo 45 vilikutwa na kasoro ndogondogo, vilipewa ushauri na viliweza kurekebisha katika kipindi kifupi na kuendelea na utoaji wa elimu ya juu.

Vyuo 19 vilikutwa na kasoro kubwa, vilipewa ushauri na muda wa marekebisho. Hata hivyo havikuweza kurekebisha katika kipindi kifupi na hivyo kuzuiwa kudahili wanafunzi wapya kuanzia mwaka wa masomo 2017/2018.

Mpaka kufikia Oktoba 2019, vyuo vikuu nane (08) kati ya 19 vilivyositishwa udahili viliweza kufanya marekebisho makubwa na hivyo kuruhusiwa kudahili na kuendelea kutoa mafunzo kwa baadhi ya programu za masomo. Vyuo hivyo ni pamoja na:

i) Chuo Kikuu cha Umoja wa Afrika Tanzania (UAUT);
ii) Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU);
iii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo – Tabora (AMUCTA);
iv) Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Tanzania (KIUT);
v) Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian (MARUCo);

vi) Chuo Kikuu Kishiriki cha Uhandisi na Teknolojia cha Mt. Yosefu (SJUCET);
vii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMUCo); na
viii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano – Moshi (SMMUCo).

## 2.0 Maamuzi ya Tume kati ya Agosti 2019 na Januari 2020

Tume imeendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhusu hali ya ubora katika vyuo ambavyo bado vilikuwa na mapungufu ya ubora. Kwa kuzingatia matokeo ya ufuatiliaji uliofanyika, Tume katika vikao vyake vya 89, 91, 92 na 97 vilivyofanyika kati ya mwezi Agosti 2019 na Januari 2020 imefanya maamuzi yafuatayo:

### 2.1. Imerejesha udahili wa wanafunzi wapya kwa Chuo kimoja (1) kuanzia mwaka wa masomo 2020/2021

Tume imeridhishwa na maboresho yaliyofanywa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisko (SFUCHAS) kurekebisha mapungufu ya ubora yaliyokuwa yamebainishwa hapo awali na kukidhi vigezo vya ubora kwa mujibu wa miongozo iliyopo. Hivyo Tume katika kikao chake cha 97 kilichofanyika tarehe 20 Januari 2020 imeruhusu chuo hicho kuanza kudahili wanafunzi wapya kuanzia mwaka wa masomo 2020/2021.

### 2.2. Imeendelea kusitisha udahili wa wanafunzi wapya kwa Chuo kimoja (1) na kutoa muda zaidi wa kutekeleza maelekezo ya Tume

Tume katika kikao chake cha 97 kilichofanyika tarehe 20 Januari 2020 imeendelea kusitisha udahili wa wanafunzi wapya kwa ngazi zote za masomo kwa programu zote kwenye Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU). Chuo hiki kimepewa muda wa miezi sita kukamilisha utekelezaji wa maelekezo ya Tume. Wakati huo Chuo hiki kitaendelea kuwa chini ya uangalizi maalumu wa Tume na hakiruhusiwi kudahili wanafunzi wapya kwenye programu zote kwa ngazi zote za masomo (kuanzia astashahada, stashahada, shahada, shahada ya uzamili, hadi Shahada ya Uzamivu).

## 2.3. Imeridhia maombi ya Wamiliki kufuta Vyuo Vikuu Vishiriki viwili (02) na Vituo Vitatu (03) vya Vyuo Vikuu

Kufuatia mashauriano na maombi yaliyofanywa na wamiliki wa vyuo vikuu vishiriki viwili (02) na Vituo Vitatu (03) vya Vyuo Vikuu kusitisha utoaji wa mafunzo, Tume katika kikao chake cha 97 kilichofanyika tarehe 20 Januari 2020 imeridhia maombi ya wamiliki hao ya kusitisha utoaji wa mafunzo, hivyo Tume imefuta Hati za Usajili za Vyuo Vikuu Vishiriki na kufuta vibali vilivyoanzisha Vituo vya Vyuo Vikuu vifuatavyo:

i) Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Yakobo (AJUCo);

ii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Kadinali Rugambwa (CARUMUCo);

iii) Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji – Kituo cha Dar es Salaam (TEKU – Dar es Salaam Centre);

iv) Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania – Kituo cha Mt. Marko (SJUT – St. Mark's Centre); na

v) Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Kilimo na Teknolojia Kituo cha Arusha (JKUAT – Arusha Centre).

## 2.4. Imefuta Hati za Usajili za Vyuo Vikuu vitatu (03) na Chuo Kikuu Kishiriki kimoja (01)

Licha ya Tume kutoa ushauri na mafunzo ya namna mbalimbali za kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, pamoja na kutoa muda wa kufanya maboresho kwenye maeneo mbalimbali yaliyobainishwa kwa zaidi ya miaka mitatu (03), baadhi ya vyuo havikufanikiwa kufanya maboresho kama inavyotakiwa. Kwa kuzingatia muda uliotolewa na hali ya vyuo husika ikiwa ni pamoja na changamoto ya uhaba wa rasilimali watu na fedha, imedhihirika kuwa baadhi ya vyuo havina uwezo wa kujiendesha hata vikipewa muda zaidi. Kwa sababu hiyo, Tume katika vikao vyake vya 89, 91, 92 na 97 vilivyofanyika kati ya mwezi Agosti 2019 na Januari 2020 imefuta Hati za Usajili za vyuo vifuatavyo:

i) Chuo Kikuu Kishiriki cha Josiah Kibira (JOKUCo);

ii) Chuo Kikuu cha Mlima Meru (MMU);

iii) Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia (IMTU); na

iv) Chuo Kikuu cha Bagamoyo (UoB).

## 3.0 Hitimisho

Tume ya Vyuo Vikuu itaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhusu hali ya ubora katika vyuo vikuu vyote hapa nchini. Aidha, Tume itaendelea kushirikiana na vyuo vikuu vyote na wadau mbalimbali wa elimu ya vyuo vikuu kwa lengo la kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango vya ubora kitaifa, kikanda na kimataifa.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa
**KATIBU MTENDAJI**

**21 Januari, 2020**